CDPH | Idara ya AFYA YA UMMA ya Chicago

# Surua (Measles): Dhana Potofu dhidi ya Ukweli

☒ ***DHANA POTOFU: Surua si ugonjwa hatari na ni "homa tu".***
☑ **UKWELI:** ***Ugonjwa wa surua unaweza kusababisha matatizo makubwa*** kama vile nimonia (maambukizo ya mapafu), encephalitis (uvimbe wa ubongo), na hata kifo, hasa kwa watoto wadogo wasipochanjwa. Makadirio yanaonyesha kuwa mtoto 1 hadi 3 kati ya watoto 1,000 walioambukizwa ugonjwa wa surua hufa.

☒ ***DHANA POTOFU: Ugonjwa wa surua umekomeshwa nchini Marekani.***
☑ **UKWELI:** Ugonjwa wa surua ulikomeshwa nchini Marekani mwaka wa 2000 kutokana na chanjo bora zaidi ya MMR na idadi kubwa ya watu waliopokea chanjo. Angalau asilimia 95 ya jamii lazima ipate chanjo ili kuzuia visa na milipuko ya ugonjwa wa surua. Kwa bahati mbaya, ***milipuko ya ugonjwa wa surua bado inaweza kutokea kwa sababu ya kupungua kwa idadi ya watu wanaopokea chanjo na kusafiri kwa watu ambao hawajachanjwa.***







☒ ***DHANA POTOFU: Mfumo wako wa kingamaradhi unaweza kukukinga usipate ugonjwa wa surua.***
☑ **UKWELI:** Ugonjwa wa surua unaambukiza sana na huenezwa kwa urahisi sana. Mtu mmoja akiwa nao, watu 9 kati ya 10 ambao hawajachanjwa wataambukizwa pia ikiwa watamkaribia, bila kujali historia ya kimatibabu au lishe. Huenezwa kupitia hewani wakati mtu aliyeambukizwa anakohoa au kupiga chafya. Virusi vya ugonjwa wa surua hubaki hewani na kwenye sehemu zilizoendewa na virusi hivyo kwa hadi saa 2 baada ya mtu aliyeambukizwa kuondoka chumbani. ***Njia bora na nzuri pekee ya kuzuia kupata ugonjwa wa surua ni kuchanjwa na chanjo ya MMR.***

☒ ***DHANA POTOFU: Ugonjwa wa surua unaenezwa na watu waliochanjwa na kliniki za chanjo.***
☑ **UKWELI:** Chanjo ya ugonjwa wa surua ina namna ya virusi hai vilivyodhoofishwa ambavyo haviwezi kuambukiza watu, na havijawahi kuthibitishwa kuwa huenezwa kwa watu wengine. Visa na milipuko ya ugonjwa wa surua husababishwa na aina hatari ya virusi vya ugonjwa wa surua, si aina ya virusi vilivyo kwenye chanjo. ***Chanjo ya MMR haisababishi ugonjwa wa surua bali hufunza mfumo wako wa kingamaradhi kutambua virusi vya ugonjwa wa surua na kujenga kinga ya kuvizuia.***

☒ ***DHANA POTOFU: Chanjo ya ugonjwa wa surua haifanyi kazi na ni hatari.***
☑ **UKWELI:** Chanjo ya MMR huzuia ugonjwa wa surua na magonjwa mengine mawili yanayosababishwa na virusi ikijumuisha matumbwitumbwi na rubela. ***Chanjo ya MMR ni bora zaidi kwa kuzuia ugonjwa wa surua ambapo dozi mbili huwa na ufanisi wa 97% na hujenga kinga ya kudumu.*** Pia, hakuna vifo vilivyoripotiwa kuhusiana na chanjo ya MMR kwa watu wenye afya. Chanjo ya MMR ni salama sana na inaweza kuwa na athari za muda ikijumuisha maumivu ya mkono (kutokana na kudungwa sindano), kuhisi joto jingi mwilini, kutokwa na vipele kiasi, maumivu/mkakamao wa muda wa viungo. Kupata chanjo ni salama zaidi kuliko kupata ugonjwa wa surua.



☒ ***DHANA POTOFU: Chanjo ya MMR husababisha ugonjwa wa akili wa watoto.***
☑ **UKWELI: *Chanjo ya MMR HAISABABISHI ugonjwa wa akili wa watoto.*** Kuna tafiti nyingi kubwa zilizofanywa vizuri zilizochunguza mamia ya maelfu ya watoto, na hazionyeshi ushahidi wowote kwamba chanjo ya MMR husababisha ugonjwa wa akili wa watoto. Hakuna kijenzi cha chanjo kinachoweza kuathiri au kubadilisha ubongo au mfumo wako wa neva.

Mabadiliko mengi ya ubongo yanayohusiana na ugonjwa wa akili wa watoto hutokea wakati mtoto anakua tumboni au wakati wa kuzaliwa, mapema kabla mtoto hajapokea chanjo. Karibu 85% ya hatari ya kupata ugonjwa wa akili wa watoto inatokana na maumbile. Ushahidi pia umeonyesha kuwa hali za mazingira zinaweza kuchangia kwa ugonjwa wa akili wa watoto, kama vile umri mkubwa wa wazazi, kuzaliwa kabla ya wakati, kuzaliwa na uzito mdogo, kuathiriwa na hewa chafu wakati wa ujauzito au dawa fulani za kuua wadudu na magonjwa ya mama, kama vile ugonjwa wa kisukari au matatizo ya mfumo wa kingamaradhi.

☒ ***DHANA POTOFU: Unaweza kuzuia ugonjwa wa surua kwa kutumia matibabu mengine kama vile vitamini A.***
☑ **UKWELI:** Hakuna hatua zilizothibitishwa za uzuiaji wa ugonjwa wa surua za lishe au mtindo wa maisha. ***Njia bora na ya pekee iliyothibitishwa ya kuzuia ugonjwa wa surua ni kupitia kupokea chanjo ya MMR.*** CDC inapendekeza watoto wote wapokee dozi mbili za chanjo ya MMR kuanzia umri wa miezi 12 hadi 15 kisha wapokee dozi ya pili wakifikisha umri wa kati ya miaka 4 hadi 6. Chanjo huchukua karibu wiki mbili hadi tatu kujenga kinga kamili. Ikiwa familia yako inasafiri nje ya nchi, zungumza na mtoa huduma wako wa afya kuhusu kupata chanjo ya MMR mapema.

Vitamini A wakati mwingine inaweza kusaidia katika matibabu ya watoto wadogo wanaopata maambukizo makali ya ugonjwa wa surua. Matibabu haya lazima yafanyike chini ya usimamizi wa mtoa huduma wa afya hospitalini, lakini vitamini A haitakukinga usipate maambukizo ya ugonjwa wa surua. Vitamini A husaidia mfumo wako wa kingamaradhi. Si tiba ya maambukizo ya ugonjwa wa surua, na haipaswi kuchukua nafasi ya chanjo ya MMR. Kutumia vitamini A nyingi kunaweza kuwa hatari zaidi na sumu na kusababisha matatizo ya neva na ini kutofanya kazi.



## ILI UPATE MAELEZO ZAIDI

Kliniki za Chanjo za CDPH hutoa huduma kwa wakazi wote wa Chicago. Unaweza kuombwa uonyeshe uthibitisho wa makazi yako.

**CHICAGO.GOV/VACCINES**

CDPH
Chicago Department of Public Health

**CHICAGO.GOV/MEASLES**

Ikiwa unahitaji msaada wa kutambua mtoa huduma mwingine wa chanjo, tafadhali tembelea:

**VFC.ILLINOIS.GOV/SEARCH/**


Marejeleo:

Casler, A. (2 Mei 2019). *Dhana 10 Potofu za Kawaida Kuhusu Ugonjwa wa Surua – na Ukweli Halisi.* Orland Health. https://www.arnoldpalmerhospital.com/content-hub/10-common-myths-about-measlesand-the-real-facts

Kituo cha Udhibiti na Uzuiaji wa Magonjwa. (17 Januari 2025). *Chanjo ya Ugonjwa wa Surua.* https://www.cdc.gov/measles/vaccines/index.html#:~:text=The%20vaccine%20is%20safe%20and,go%20away%20on%20their%20own.

Children's Hospital Colorado. (11 Machi 2025). *Ukweli Kuhusu Ugonjwa wa Surua kwa Watoto: Mambo Ambayo Wazazi Wanahitaji Kujua.* https://www.childrenscolorado.org/just-ask-childrens/articles/measles/#:~:text=Despite%20myths%20and%20misinformation%2C%20vaccines,number%20of%20cases%20in%202024.

Shirika la Marekani la Magonjwa ya Kuambukiza. (8 Aprili 2025). *Chanjo ya Ugonjwa wa Surua: Jua Ukweli.* https://www.idsociety.org/public-health/measles/know-the-facts/

Taasisi ya Kitaifa ya Sayansi za Afya ya Mazingira. (1 Aprili 2025). *Ugonjwa wa Akili wa Watoto.* https://www.niehs.nih.gov/health/topics/conditions/autism